JIMBO KU U KATOLIKI LA DAR ES SALAAM
PAROKIA YA MOYO MTAKATIFU WA YESU MANZESE
Barua pepe : parokiamanzese@gmail.com
S. L. P. 55095

HITORIA FUPI YA PAROKIA YA MOYO MTAKATIFU WA YESU MANZESE

Miaka ya 1963 na 1964 eneo la Manzese lilikuwa linaitwa 'SOWETO' ikimaanisha kwamba kilikuwa kitovu cha kila aina ya uovu mathalani ulevi wa kupindukia,uasherati,uvutaji bangi,ujambazi na kadhalika.Mazingira kama haya yalihitaji neno la Mungu ambalo ni mwanga kama alivyosema Yesu mwenyewe kuwa '**Mimi ndimi nuru ya ulimwengu,yeye anifuataye hatakwenda gizani kamwe"(Yohana 8:12)**

Ilionekana kwamba kulikuwa na hitaji la kupanda mbegu ya neno la Mungu katika maeneo ya Manzese.Hivyo basi mwanzoni Ushirika wa Moyo Mtakatifu wa Yesu ulihusika sana katika kuanzisha harakati za kusambaza neno la Mungu katika eneo la Manzese.Mwanzoni kabisa ushirika huu ulijitokeza kwa kununua nyumba ya vyumba sita katika eneo ambalo kwa sasa linaitwa Tip Top ambamo mikutano ya wakristu ilikuwa inafanyikia.Chama cha Moyo Mtakatifu wa Yesu kwa kushirikiana na chama cha Lejio Maria walihakikisha injili inahubiliwa mahali pote katika vilabu vya pombe,mitaani na majumbani.Mpaka kufikia mwaka 1969 ikaonekana kwamba upo umuhimu wa Parokia ya Magomeni kuhudumia wakristu wa Manzese kwa Misa Takatifu.Wakati huo nyumba ya ushirika ilionekana ndogo wakaamua kutumia jumba la baa ya Pombe ikawa jumba linasafishwa mapema kabla ya ibada ya misa Takatifu .Mazingira haya hayakutosheleza ndipo ushirika wa Moyo Mtakatifu waliamua kuvunja nyumba hiyo ya vyumba sita na kuamua kujenga kikanisa kidogo na kuanza kueneza injili kwa kasi.

Wakati imani inaanza kupandwa katika sehemu ya Manzese tukiwa chini ya Parokia ya Magomeni,tukilelewa na Mapadre wa Shirika la Wafransisco – Wakapuchini wakati huo Baba Baba Paroko alikuwa Padre Oswin na msaidizi wake Padre John G.Menezes na wengine kama Padre C.Luoga ,Cosmas na wengineo.

Tarehe 01/04/1978 Mwadhama Lauriano Kadinali Rugambwa alizindua rasmi Parokia yetu ambapo Parokia ilichagua Moyo Mtakatifu wa Yesu kuwa msimamizi wa Parokia ikiwa ni kuonyesha ukarimu na shukurani kwa Bwana wao na kumwomba ili azidi kuendelea kuwaongoza katika Imani na Upendo.

Mara baada ya uzinduzi wa Parokia Mwadhama Kadinali Lauriano Rugambwa alimwomba mkuu wa shirika la Wamisionari wa Afrika(White Fathers) Padre JOHN HEIGH ambaye alikuwa mkuu wa shirika tawi la Tanzania kuendesha Parokia.Mkuu wa shirika alikubali ombi la Mwadhama Kuendesha Parokia ya Manzese.Shirika lilitoa mapadre watatu kuendesha Parokia ambao **ni Baba Paroko Padre Gerald Nolf(Marehemu),wasaidizi Padre Charles Matte(Marehemu) na Bernado Amersvoot(marehemu) hawa ndiyo waasisi wa Parokia ya Moyo Mtakatifu wa Yesu Manzese**

Wakati Parokia ya Moyo Mtakatifu wa Yesu Manzese inaanzishwa mwaka 1978 pamoja na kuwa na mapadre watatu Parokia pia ilikuwa na viongozi Walei ambao walikuwa ni Mwenyekiti ndugu Francis Chawangula,Makamu mwenyekiti ndugu Costa Rwegarulila,Katibu ndugu Eva Tarimo,Katibu msaidizi Paulo Ifunya na Mwekahazina ndugu Raulent Kwembe

Shirika la Wamisionari wa Afrika (White Fathers) wameongoza Parokia ya Moyo Mtakatifu wa Yesu kwa miaka isiyopungua 38 mpaka tarehe 01/05/2019 ndipo Parokia yetu ilitangazwa rasmi kuwa chini ya Jimbo kuu la Dar es salaam.Uongozi wa Jimbo kuu la Dar es salaam kwa mara ya kwanza ulimleta Baba Paroko Theophil Bolampet akisaidiwa na Padre Garren Mvungi na baadaye aliletwa Padre Cretus Mzeru.

Parokia kwa sasa inaongozwa na **Baba Paroko Padre Benedict Shayo, Paroko msaidizi ni Padre Paulo Sabuni na viongozi wa kamati Tendaji ya Parokia ni Mwenyekiti ndugu Protasi Mbena,Makamu mwenyekiti Mama Adelhaida Komba,Katibu ndugu Adrian Msilikale,katibu msaidizi ndugu Abdon Moshi,na Mwekahazina ni Melkizedeki Mallya.**

Mafanikio

Tangu kuanzishwa kwa Parokia yetu mafanikio mbalimbali yamepatikana ambapo mpaka sasa Parokia ina waumini wasipungua 4000 kutoka katika Jumuiya 57 na kanda 13 ambazo ni Kanda

yaEmausi,Maghorofani,Kilimani,UbungoPlaza,Msufini,Mvuleni,Uzuri,Ukombozi,Darajani,Engo ,Mpakani,TipTop,Msufini na Kanda ya Wageni

Kiroho,Yapo mafanikio makubwa kwa waumini wetu kama ifuatavyo:Waumini wengi wamepokea masakramenti mbalimbali kama ubatizo,komunio,kipaimara,ndoa,mpako wa magonjwa,Misa za mazishi,kutembelea wagonjwa ,kusaidia wasiojiweza,kubariki nyumba za waumini,kushiriki maadhimisho mbalimbali yanayoratibiwa na Jimbo kuu la Dar es salaam.

Elimu,Parokia inaendesha shule ya awali ambayo kwa sasa iko chini ya Jimbo kuu la Dar es salaam, pia kuna chuo cha Ufundi wa ushonaji kilichosajiliwa na VETA kwa ajili ya wanafunzi wanaomaliza elimu ya msingi na watu wazima wanaotaka kujifunza kushona.Pia kwa kutumia mfuko wa MEMA Parokia imekuwa ikiwapatia karo na matumizi mengine vijana wanaoishi katika mazingira magumu kuanzia chekechea mpaka masomo ya juu.

Afya,Kupitia kamati ya afya Parokia imeendelea kushauri katika kuboresha mazingira ya Parokia na kutoa huduma mbalimbali kama upimaji wa VVU,Upimaji wa macho na upatikanaji wa Bima ya afya kwa waumini.

Karitasi,Kupitia kamati ya karitasi Parokia imeendelea kutoa msaada kwa waumini na watu wasiojiweza kwa kuwapatia mahitaji mbalimbali ikiwemo chakula,mavazi na misaada mingine kulingana na mahitaji yao.

Kijamii,Parokia tangu kuanzishwa kwake imeendelea kuwa na mahusiano na ushirikiano mzuri na taasisi mbalimbali zilizopakana na Parokia Yetu.

Vyama vya Kitume,Parokia yetu inavyo Vyama mbalimbali vya Kitume kama Moyo Mtakatifu wa Yesu,Lejio Maria,Karismatiki katoliki,WAWATA,UWAKA,Msamaria mwema,Watumishi wa Altare,VIWAWA,Shikwaka,Utoto Mtakatifu,Chama cha Wito,Mtakatifu Anna,Wajane,Wasomaji masomo kanisani na Vifra.

Kamati za Parokia,Pia Parokia yetu inazo kamati mbalimbali zinazosaidia katika shughuli mbalimbali za utume hapa Parokiani kama Kamati ya Afya,Kamati ya Ulinzi,Kamati Karitasi,Kamati ya Elimu,Kamati ya Fedha na Uchumi,Kamati ya Liturujia,kamati ya Familia na malezi na Kamati ya Ardhi.

Hitimisho,Parokia yetu tarehe 01/04/2018 ilifikisha miaka 40 tangu kuanzishwa kwake na katika kumshukuru Mungu Parokia ilifanya Jubilei ya miaka 40 ambapo wanaparokia kwa pamoja walisherekea kwa kula na kunywa pamoja lakini zaidi kumshukuru Mungu.Katika Jubilei hiyo Parokia ilitekeleza mambo mbalimbali kama ujenzi wa Grotto ya Moyo Mtakatifu wa Yesu,kukarabati Grotto ya Mama Bikira Maria,Kupaka rangi kanisa.Waumini zaidi ya hamsini ambao walikuwa wanaishi bila kufunga ndoa walifunga ndoa,Pia kulikuwa na Sakramenti ya Ubatizo kwa zaidi ya watoto 100,Komunio ya kwanza na Kipaimara.

TUMSIFU YESU KRISTO……